

COVID-19 | Maatregelen | 02/11/2020

Swahili | Vertaald uit het Nederlands

## Hatua za tarehe mbili novemba

### Utangulizi

Serikali imechukua misimamo za kuzuia kusambaa kwa janga la virusi ya corona. Heshimuni hatua hizo. Na hivi basi, tuepuke kupata magonjwa hayo na kuambukiza watu wengine. Polisi inahusika nakuchunguza heshima ya misimamo hizo.

Angalisho : Jiji na mitaa zimoja zimechukua vilevile misimamo ya ziada. Kwa maelekezo zaidi, chunguza tovuti ya mji au ya mtaa wako.

### Kanuni sita ya msingi

- Nawa mara na mara mikono yako kwa maji na kwa sabuni.
- Vaa barakoa yako au mask.
- Heshimu kwa kiwango cha chini, mita moja na nusu ya kutengana na wengine mukiwa pamoja.
- Mawasiliano ya karibu inaruhusiwa na mtu mmoja tu, Kwa hiyo si lazima kuheshimu umbali wa mita moja na nusu ukiwa na mtu wako wa karibu.
- Shurulikia hasa (zaidi) watu wenye kasoro :
  - Watu ambao wana umri wa miaka zaidi ya sitini na tano
  - Watu ambao wana shida za moyo, za mapafu na za figo.
  - Watu ambao wanaweza pata maambukizi haraka.
- Tumikia nyumbani.
- Ingiza hewa vizuri : fungua madirisha.
- Ni heri zaidi mikutano zifanyike nje (au pendelea zaidi mikutano za nje)

### Kusafiri kwenye jiji lingine au ugenini

- Ubeljiji :
  - Unaweza safiri huru.
  - Unatumia uchukuzi wa pamoja (basi, tremu, gari la moshi) ? Unazaidi ya miaka kumi na mbili ? Unapashwa kuvaa barakoa (mask) ao kitambaa yenye kufunika vizuri kwa pamoja kinywa na pua. Hiyo ni sharti inatiwa mkazo kwa watu wote.
  - Haupashwi patikana barabarani kati ya usiku wa manane (minuit) na saa kumi na moja ya asubui.
- Ugenini :
  - Ni vema zaidi kutosafiri ugenini. Hiyo ni shauri.
  - Ni lazima tu ujielekeze ugenini ? Fahamu ya kwamba kuna aina tatu za eneo.

- ▶ Unaweza safiri kwenye eneo ya kimajani. Hiyo siyo hatari.
  - ▶ Inakatazwa kusafiri kwenye eneo nyekundu au ya machungwa.
  - Tembelea (fungua) tovuti ya wizara ya mambo ya nje (Affaires Etrangères) : <http://diplomatie.belgium.be>.
  - Misimamo zinaweza badilika kufuatana na nchi. Utazipata kwenye mtandao : [https://diplomatie.belgium.be/fr/Services/voyager\\_a\\_lettranger/conseils\\_par\\_destination](https://diplomatie.belgium.be/fr/Services/voyager_a_lettranger/conseils_par_destination)
  - Unaweza kujaza hati (ama fomula, kizibo) kabla ya kurejea (ama kurudi) nchini Ubeljiji. Utapata tupu hii kunako : <https://travel.info-coronavirus.be/fr/public-health-passenger-locator-form>
  - Ulibaki kwenye eneo nyekundu kwa muda ya zaidi ya saa makumi mane na nane ? Ni lazima ufanye mambo tatu zifuatayo wakati unarudi Ubeljiji :
- 1 Jaza hati (ama fomula, kizibo) kwenye: <https://travel.info-coronavirus.be/fr/public-health-passenger-locator-form>.
  - 2 Unapokea ujumbe mfupi (texto)? Unapashwa kujitia katika karantini. Unapashwa baki nyumbani kwako mnamo muda wa siku kumi kwa kiwango cha chini. Usitoke nyumbani, isipokuwa tu kama ni lazima (muhimu) sana. Kwa mfano: kujielekeza kuona mchanganyaji dawa (mfamasia), daktari ama kwenye duka kubwa. Vaa wakati wowote barakoa (mask) yako.
  - 3 Haupokei ujumbe mfupi (texto)? Haupashwi (haulazimishwi) kujitia katika karantini.

### Kazi

- Tumikia nyumbani kwako. Hiyo inawajibika (au ni sharti)
- Ni lazima kwenda offisini ?
  - Unapashwa kuvaa barakoa au mask yako.
  - Ingiza hewa vizuri : fungua madirisha.
- Una ulizo ? Mwajiri wako atakujibu (atakusaidia ).

### Biashara

- Maduka za muhimu (za lazima) zimefunguliwa. Kwa mfano : duka kubwa, tanuri ya mikate, duka ya dawa au posta. Vituo vya bustani, maduka ya vitabu na maduka la ufundi au ya kazi ya mikono (bricolage) zimefunguliwa vilevile.
  - Munaweza fanya dharura mukiwa watu wawili tu kwa kiwango cha juu.
  - Muda wa dharura ni wa dakika thelathini (makumi tatu) tu kwa kiwango cha juu.
  - Vaa barakoa au mask yako. Hiyo ni sharti inatiwa mkazo kwa watu wote.
- Maduka zingine zote zimefungwa. Ila unaweza chukua au kutolea toleo yako.
- Maduka za usiku zimefunguliwa hadi saa inne za usiku.
- Auruhusiwi kununua pombe ya kulevya baada ya saa mbili ya usiku.
- Mahali pa kunyolea na zile ya kutengenezea nywele zimefungwa.

### Sekta ya hoteli na upishi

- Mahali pa kuuzishia pombe na migahawa (ama restorenti) zimefungwa.
- Unaweza nunua vyakula vya kubeba nyumbani hadi saa inne ya usiku.

### Mawasiliano za Kijamii

- Unaweza kua na mawasiliano ya karibu na mtu mmoja akiwa uleule kwa kiwango cha juu. Aulazimishwi kuheshimu umbali wa mita moja na nusu. Watoto wa umri ya miaka chini ya kumi na mbili hawahesabiki.
- Unaalika mtu nyumbani kwako ? Unaweza alika tu mtu mmoja wa karibu kwa jamaa.
- Unaishi peke yako ? Unaweza alika mtu wako wa karibu na mtu mwingine umoja nyumbani kwako. Watu hawa hawapashwi kujikuta kwako kwa wakati moja.
- Munakusanyika barabarani ? Idadi inayoruhusiwa aipashwi tambuka watu inne kwa kiwango cha juu. Munapashwa heshimu umbali wa mita moja na nusu.

### Mazoezi

- Unaweza fanya michezo nje katika kundi lisilo tambuka hesabu ya watu manne kwa kiwango cha juu. Uheshimu umbali wa mita moja na nusu kwa kujitenga na wengine.
- Klabu za michezo, nafasi ya kuongelea, vituo ya afya bora na vituo ya uzima zimefungwa.

### Burudani

- Mambo yote yamefungwa, kwa mfano, sinema, kasino, wanja za kivutio na bustani za wanyama.
- Akuna andaliwa hata tukio fulani wala tamasha. Kwa mfano : ukumbi wa michezo au tamasha ( konsati).
- Maktaba zinabaki wazi.
- Wanja za michezo za nje zinabaki wazi.
- Bustani ya likizo zinafunga tarehe tatu novemba. Nafasi za kuongelea, migahawa (ama restorenti) na fasi za kupumzikia za bustani zimekwisha tayari kufungwa.

### Dini

- Ibada za kidini aziruhusiwi (au akuna ibada ya kidini ambayo itafanyika)
- Mahali za sala zinabaki wazi (au zinafunguliwa).
- Mikutano inapunguzwa hadi watu inne.
- Heshimu umbali wam ita moja na nusu.
- Unapashwa kuvaa barakoa yako au mask.
- Mazishi inaweza pokea watu kumi na tano. Akuna chakula ambayo watu watachangia baada ya mazishi.
- Ndoa zinaweza andaliwa. Hiyo inaruhusiwa tu kwa wanandoa., mashahidi wawili kwa kiwango cha juu, afisa wa serikali, muhusika au mwenye kuhusika na ibada (kwa mfano padri au Iman (Shee)).

### Hori na masomo au mahali ya ulinzi ya watoto na shule

- Hori au mahali ya ulinzi ya watoto zimefunguliwa.
- Majifunzo imesimamishwa hadi tarehe kumi na tano novemba. Shule lako litakutolea taarifa Zaidi.

## Faraja

Misimamo ama hatua hizi ni za lazima kwa kukinga afya ya umma. Kila mmoja analazimishwa ku-ziheshimu.

Asante kwa mchango wako. Kwa pamoja, wote tunagombanisha janga la virusi ya corona.